# BARUA KUTOKA NCHI YA MBALI

Najua utafurahi kusikia hadithi ya Abdul Qadir. Kabla ya Abdul Qadir kufikisha umri wa miaka miwili wazazi wake walikufa. Walimwachia kija- na wao mali nyingi na nyumba kama urithi wake. Baba yake mkubwa alichaguliwa kuwa rnlezi wake na mali aliyorithi. Utaratibu huu ungekuwa mzuri sana katika mazingira ya kawaida.

Lakini ilitokea kwamba Baba yake mkubwa alikuwa mtu mwovu sana. Alimpeleka katika nchi ya mbali kwa jamaa yake mwingine ambaye pia hakumjali sana huyu kijana. Na yule baba yake mkubwa akasambaza habari kuwa Abdul Qadir amekufa. Akauza ile mali na kutumia fedha kwa mahitaji yake binafsi. Kadri Abdul Qadir alivyokuwa akikua, alifahamishwa kuwa yeye alikuwa yatima, masikini na asiye na kwao, tegemezi kwa watu wakarimu. Tokea wakati huo, alilazimika kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maisha yake. Kutokana na hali hii hakuweza kujifunza vizuri kusoma na kuandika.

Miaka nayo ilizidi kuenda, mara Abdul Qadir akafikia umri wa miaka ishirini na mbili. Siku moja, saa za jioni alipokuwa peke yake nyumbani, alipokea barua ambayo ilikuwa na anwani ya jina lake. Unaweza kufikiria furaha yake – barua yake! Baada ya kurudi mashambani siku ya pili yake, bila ya kutaka kuonekana na mtu akaifungua barua yake na kuanza kusoma kwa shida sana. Barua hiyo ilikuwa na ujumbe huu:

*Kwa mheshimiwa Abdul Qadir, mwana wa Mubarak:*

*Amani iwe nawe. Mimi mwandishi wa barua hii, ni Abdul Aziz, Mjomba wako. Miaka kadhaa iliyopita, nilisikia yale yaliyokukuta na kuwa bado uko hai. Nafurahi kwamba bado uko hai, kwa maana wewe ni nyama ya nyama yangu na damu ya damu yangu. Moyo wangu wakufurahia sana.*

*Mpendwa Abdul Qadir, bila shaka hujui kwamba upo katikati ya maadui, ambao wamekuibia urithi wako, ambao uliachiwa na baba yako. Nimenuia kuununua tena uritihi wako ili niurudishe tena uwe wako. Baada ya miaka mingi ya mahangaiko na mateso, nimelipa gharama hiyo kubwa na sasa mali hiyo kubwa iko mikononi mwangu. Stakabadhi iko mkononi mwa Qadhi (Jaji wa Mahakama ya Kiislamu), ambaye Jina lake nimeambatanisha. Hati inahitaji tu sahihi yako ili mali hiyo iwe yako. Hivyo peleka barua hii kwa Qadhi, ukajitambulishe mwenyewe na tutakapokutana katika siku za usoni tutafurahi pamoja.*

Abdul Qadir alikuwa hajawahi kusikia jambo la namna hii hata siku moja maishani mwake; na hivyo hakujua aamini nini. Je, yeye alikuwa mtu maskini aliyehitajika kufanya kazi kama mtumwa kwa ajili ya kipande cha mkate kwa maisha yake yote? Au kweli yeye alikuwa mrithi wa utajiri mkubwa? Hakumbuki ni mara ngapi aliisoma ile barua, kutokana na furaha kubwa aliyokuwa nayo. Hatimaye akaificha barua hiyo chini ya jiwe ili isije ikaonekana na mwajiri wake.

Siku ya pili asubuhi akamwambia mwajiri wake kila kitu. Yule bwana alikasirika sana. "Wewe ni mpumbavu sana!" alisema. "Hivi wewe unafikiri ndiye Abdul Qadir pekee humu duniani? Barua hii ilikuwa ni ya Abdul Qadir mwingine na wala si wewe". Yule kijana alimjibu: "Inawezekana kuwa hivyo; lakini bado jina langu limeandikwa katika barua. Nitasafiri mpaka mahali pale ili nijue ukweli wa jambo hili, hakuna shida hata likitokea jambo lolote".

Bwana wake alijaribu kila njia kumshawishi Abdul Qadir amwonyeshe ile barua, lakini vitisho vyote havikuambulia kitu. Kabla ya jua kuchwa Abdul Qadir alirudi mahali pake alipokuwa ameficha ile barua kwa siri. Akaisoma tena ile barua. Usiku ule baada ya chakula cha jioni, wanakijiji kadhaa waliokula chakula cha jioni na bwana wake walizungumza na Abdul Qadir. "Kijana, walisema, "tusikilize na ukubali hekima yetu. Usiiamini hiyo barua iliyokuja kwako.

Kuna anayetaka akusaliti kwa njia ya ujanja. Hiyo barua ni njama na sahihi yake imegushiwa. Lete hiyo barua na sisi tutakuthibitishia ukweli huu". Kwa mara nyingine tena Abdul Qadir alikataa. Ingawa wazee wale walikasirika, waliona kabisa kwamba hawana jingine lolote wanaloweza kufanya kwa wakati huo.

Bado, yale maneno ya wale wazee yalileta mashaka katika moyo wa Abdul Qadir. Je, iwapo wanayosema ni ya kweli? Akaamua kuulizia juu ya jambo hili siku ya pili asubuhi alipoenda sokoni. Baada ya udadisi mkubwa akampata mtu aliyejua mahali barua ilikotoka. Mwaka mmoja tu uliopita mtu huyu alikuwa ameutembelea mji huo. Mtu huyu akamwambia Abdul Qadir: "Katika mji huo kuna mtu anayeishi anayeitwa Abdul Aziz. Kila mtu pale mjini anazungumza juu ya wema wake na tabia yake njema. Wanasema kwamba alikuwa mtu tajiri sana; lakini katika miaka ya karibuni amekuwa akiishi kama maskini, akitaabika na kuweka akiba mali yake kwa ajili ya kusudi la ajabu".

Ilionekana kwamba kusudi la Abdul Aziz la kujisumbua hivyo halikuwa wazi kwa mtu aliyekuwa akizungumza na Abdul Qadir. Lakini Abdul Qadir alielewa! Moyo wake ukashikwa na matumaini ya furaha ambayo hajawahi kuiona katika maisha yake yote. Alijua kusudi la masumbuko ya upendo ya Abdul Aziz, Ilikuwa ni kwa ajili yake, Abdul Qadir!

Kwa mara nyingine tena Abdul Qadir alimweleza mwajiri wake kwamba anataka kusafiri kwenda katika nchi ile. Bwana wake akamtishia tena, akisema kwamba atamweka jela. Na alifanya hivyo. Lakini Mungu alikuwa pamoja na Abdul Qadir.

Usiku Abdul Qadir alifanya kazi ya kuchimba shimo chini ya ukuta, na kutoroka. Usiku ule ulikuwa na mbalamwezi aliichukua barua yake na akaanza kuelekea katika mji wa Abdul Aziz. Alijificha mchana na kusafiri wakati wa usiku mpaka alipokuwa mbali kabisa na mwajiri wake. Aliisoma barua yake tena na tena akiwa safarini! Ilimpa matumaini na furaha. Baada ya majuma kadhaa ya safari na kuulizia ulizia, alifika katika ule mji na kuiona nyumba ya Qadhi. Qadhi alipofungua mlango, alimwona kijana ambaye alionekana kama mrithi wa mali hiyo kubwa! Abdul Qadir aliuza kila alichokuwa nacho ili kununua chakula alipokuwa safarini. Mwili wake ulifunikwa na matambara machakavu na amiguuni alikuwa pekupeku. Bado Qadhi aliridhika Abdul Qadir alipojitambulisha na kumwonyesha ile barua. "Umefanya vizuri", alisema. "Abdul Aziz hakutaka kukulazimisha uje. Alipenda sana kukuona kama utaamini ahadi yake na kuwa na moyo wa kufanya safari. Sasa kwa kuwa umekuja, tutakamilisha hati mbele ya mashahidi. Na ndipo utamiliki mali yako".

Abdul Qadir alipolala usiku ule, unaweza kufikiria alijisikiaje? Maana sasa alikuwa na hakika kwamba haikuwa ndoto. Yeye ndiye aliyekuwa mwenye mali yote pamoja na nyumba! Na aliahidi kufanya kila awezalo kutunza ile mali.

Hakuna haja ya kukueleza ni jinsi gani Abdul Qadir alivyokuwa toka wakati huo na jinsi alivyokuwa akitembea na kuangalia uzuri wa mali aliyomiliki. Zaidi ya yote jinsi alivyokuwa na hamu ya siku ile atakapokutana na Abdul Aziz, kwa sababu asingeliweza kusahau kwamba ilikuwa ni Abdul Aziz aliyetoa mali yake na kumpa yeye. Kwa hakika alimheshimu mwokozi zaidi kuliko aliyeokolewa!

*Wapendwa, kuna barua iliyokuja toka nchi ya mbali kwa ajili yako pia. Barua hii ni Injili Takatifu imekuja toka mbinguni. Inakuambia juu ya habari ya urithi ambao Mungu ameuandaa kwa ajili yako. Urithi huu hauharibiki kama urithi mwingine wa kidunia, ambao unapita, lakini huo ni halisi, kamili na wa milele.*

*Kati ya hazina hizi za milele ni pamoja na msamaha wa dhambi, wokovu, maisha mapya na amani na Mungu. Je, unajua kwamba Mungu amekuridhia urithi huu wa kimbingu kwako wewe na wanadamu wote?*

*Barua hii pia inakuambia jinsi gani Mungu amekuandalia urithi mkubwa. Inakuambia jinsi Mungu alivyomtuma Yesu Masihi ateseke kwa ajili yako. Masihi ameacha utajiri na utukufu wa kukaa na Baba yake mbinguni na kujitoa kwa ajili Yako Amekuja hapa duniani kama mwanadamu ili kuyatoa maisha yake kwa ajili yako. Ufufuko wake toka mauti ni uthibitisho wa Mungu kwamba urithi huo kwa kweli ni wako.*

*Lakini ni kwa nini Masihi alifanya hivi kwa ajili yako? Ni kwa sababu, kama jinsi barua hii inavyoeleza, umo mikononi mwa adui. Shetani amejaribu kuiba urithi wako. Anataka akuweke katika giza na ujinga kwa ajili ya urithi huu ili usijue lolote, kwa sababu Mungu anakupenda, Masihi ameteseka kuokoa urithi wako na kukuweka huru kutoka vifungo vya Shetani.*

*Mpendwa, Je, una imani na ahadi hii ya Mungu? Je, unao moyo wa kuacha maisha yako ya kale ya dhambi na utumwa kwa Shetani? Uko tayari kupokea zawadi kubwa ambayo Mungu anataka kukupa?*

*Bila shaka kuna watu wengine watakaokukatisha tamaa. Watakuambia uendelee kubaki katika hali yako ya kale. Wengine watakuambia kwamba hiyo barua, Agano Jipya, ni kwa ajili ya mtu mwingine na si kwa ajili yako. Na wengine watasema kwamba barua yenyewe si halisi; na kwamba ujumbe wake si wa kweli, na ahadi zake ni ulaghai.*

*Hata hivyo, mpendwa barua hii imetumwa kwako, kwani ni kwa ajili ya wenye dhambi wote. Isome kwa uangalifu na kwa moyo ulio wazi. Unapoona kweli yake na kugundua thamani ya urithi huu wa milele, moyo wako, kama ule wa Abdul Qadir, utafurahi kwa ajili ya urithi wako mpya. Utakuwa tajiri katika kusamehewa, na amani na katika maisha mapya katika Masihi ambaye alikushindia. Na utangojea kwa hamu kubwa nafasi ya kumwona Masihi, kumshukuru na kufurahi naye atakaporudi tena hapa duniani kutoka mbinguni.*

*Mungu ni mkuu! Msifuni Mungu afanyaye mambo yote sawa!*

Ikiwa unapenda kujifunza zaidi juu ya Yesu Masihi, tuko tayari kukutumia vijitabu vya kukusaidia zaidi:

‘Jitahidi Kulinganisha’
Kuwa mwumini kwa hiari

Tafadhali andika jina lako na anwani ya barua pepe vema, kisha utume kwa:

info@lifechallenge.de